

HISTORIA YA MAISHA YA MSICHANA WA MIAKA TISA KUTOKA UHISPANIA.



Maria Del Carmen Gozalez - Valerio alizaliwa mjini Madrid nchini Uhispania mnamo tarehe 14 Machi mwaka 1930. Alikuwa mtoto wa pili katika familia

ya watoto watano familia ambayo ilikua imejitolea kuitumikia kanisa katoliki.

Wazazi wake walimsadiki kwa Mungu kabla ya kumzaa na baadaye kufuata wito huu wa kumsadiki kwa Mungu kila

mara walipotembelea dhabahu la Marian (shrine), pahali patakatifu.

Mungu alitaka kumfanya wake kwa kuwa alibatizwa masaa machache baada ya kuzaliwa. Alitawaswa akiwa na umri wa miaka miwili kuwa mtume nakutoka wakati huo akawa kielelezo cha wito, sadaka na majitoleo katika maisha ya utume na akaonyesha dalili za utume jambo ambalo si kawaida na laweza fafanuliwa tu kupitia neema.

Alijitosa kimasomaso kushuhudia upendo wa Kristo na alikua na hamu kubwa ya kumkaribisha Yesu kwa Ekaristi katika kiroho kupitia komuno ya kwanza kwa matamano makubwa jambo ambalo ni nadra sana kwa mtoto kama yeye. Hili lilitukia Juni tarehe 25 mwaka wa 1936 akiwa na miaka Sita pekee.

Alijisadaka kwa Kristo Yesu na Yesu akawa ni yote maishani mwake.

Alijitosa kwa utume na utakatifu ulikua unamwilishwa katika huduma. Alionyesha upendo na mshikamano sanjari na kuwajali pamoja na kuguswa na mahangaiko ya wengine kwa kutumia akiba yake katika kuinjilisha. Hangetengana na ukweli na ukweli ukawa yeye hata kwake binafsi hata kama angepata madhara au kupitia majaribu na mateso.

Alishukuru lolote alilotendewa na ilikua chanzo cha raha na furaha kwa wengine. Alikuwa mchangamfu, mchapakazi na alijidhibiti na mara nyingi kuajibikia vitendo vyake, alikuwa mwenye furaha na makini kwa kazi yake.

Alikuwa na imani thabiti iliyokuwa mwongozo na msingi katika maisha yake na hata akiwa mdogo alielewa kuwa utakatifu ni kufuata Kristo na

kubeba msalaba. Aliyakita maisha yake katika huduma na upendo. Alishuhudia, kuiga na kuyafuata yote aliyoyaona kwa kila mtu akionyesha mapenzi kwa wote.

Kubwa zaidi ni wakati alionyesha nia yakujisadiki katika kuhudumia kanisa Katoliki. Upendo wake ulifikia upeo wa juu alipojisadiki kwa waliomuua babake tarehe 29 Augusti 1936. Alijitoa sadaka Alhamisi 6 Aprili 1939 huko Maunday baada ya kumkubali Yesu kwa kula mwili wa kiroho lakini hakuna aliyejua na kuiweka siri hadi alipoaga dunia.

Yesu Kristo alikubali mwito na sadaka yake na alikufa kwa kuteseka sana tarehe 17 Julai 1939 bila malalamishi au yeyote kuteta juu yake akiwa mtiifu mpaka kufa kwake akiwataja majina Yesu, Maria na Yusufu.

Alikuwa ametabiri kifo chake na siku Mungu angekuja kumchukua kumpeleka kuzimu peponi. Na hivyo ndivyo kifo chake kilitokea na kuonekana na wale waliokuwa naye dakika za mwisho za kufa kwake.

Alikuwa mteule, mtakatifu akiwa na umri wa miaka tisa.

SALA ZA KUOMBA NEEMA KWA MWANA HERI MARIA DEL CARMEN GOZALEZ-VALERIO.

YESU ULIYESEMA, "WACHENI WATOTO WAJE KWANGU",
NA ULIKUA UNATAKA KUWEKA
ROHO YA MARIA DEL CARMEN GOZALEZ KUTUKUKA NA
KUTOJUA YA ULIMWENGU NA
KUFA BADALA YA KUFANYA DHAMBI, KWA MAPENZI
ALIYOYAWEKA NA KUDUMISHA
IMANI KWA KUJISADIKI KWAKO LICHA YA KUTESEKA
,TUNAOMBA UINGIE KATIKA
FAMILIA ZA WAKRISTO ROHO ZAO ZIKUFUATE. KAMA NI
MAPENZI YAKO KUTUKUZWA
HAPA DUNIANI, TUJALIE KUPITIA KWAKE NA NEEMA
TUNAOMBA KUTOKA
KWAKO.....

[Tafsiri kwa lugha ya kiswahili kutoka kwa Charles Ndung'u / Translated into Swahili by Charles Ndung'u / Traducido al suajili por Charles Ndung'u]